# Usimamizi wa misitu na MKUHUMI Tanzania

## Sera ya Taifa ya Ardhi na Misitu, Tanzania

Katika miaka ya karibuni kumekuwa na changamoto nyingi za uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa miti na ufyekaji wa misitu. Kufuatia hali hiyo, kumekuwa na mabadiliko mbalimbali ya kisera na kisheria hapa Tanzania yanayotoa fursa ya kuwashirikisha wananchi katika usimamizi wa rasilimali za maliasili zilizopo katika maeneo yao. Sera ya Taifa ya Misitu ya mwaka 1998 na Sheria ya Misitu ya mwaka 2002 inaelekeza kuwawezesha wananchi kutenga maeneo ya vijiji vyao na kuanzisha Misitu ya Hifadhi ya Vijiji. Aidha, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 nayo inaruhusu kijiji kutenga maeneo katika ardhi ya kijiji kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

## Nafasi ya misitu katika mabadiliko ya tabia ya nchi

Hivi sasa dunia inakabiliwa na tatizo la mabadiliko ya tabia ya nchi. Mabadiliko haya yameendelea kuleta madhara mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubadilika kwa misimu ya mvua na ukame wa muda mrefu kuongezeka kwa joto duniani n.k. Mabadiliko haya yamesababishwa na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji wa gesi joto ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa hewa ukaa itokanayo na uharibifu wa misitu.

Katika kukabiliana na tatizo hili, Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa ukaa kutokana na ukataji miti ovyo na Uharibifu wa Misitu (kwa kifupi MKUHUMI) unajadiliwa hivi sasa duniani. Mkakati huu, ambao Tanzania pia inashiriki katika majadiliano, utasaidia kuleta motisha kwa jamii zinazoshiriki kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na ukataji miti ovyo na uharibifu wa misitu.

# Mradi wa MKUHUMI kwa ajili ya jamii na uhifadhi wa misitu

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali mradi wa "MKUHUMI kwa ajili ya Jamii na Uhifadhi wa Misitu" umeanza kutekelezwa kwa majaribio katika Wilaya ya Lindi vijijini, Kilosa na Mpwapwa. Mradi unatekelezwa na mashirika ya TFCG na MJUMITA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama CARE Tanzania, Jumuiko la Maliasili Tanzania (TNRF), Clinton Foundation, Chuo kikuu cha Sokoine cha kilimo na wengine.

## Lengo kuu la mradi

Kupunguza uzalishaji wa gesijoto unaotokana na ukataji na uharibifu wa misitu Tanzania katika njia ambazo zitatoa motisha wa haki wa moja kwa moja kwa jamii vijijini kuhifadhi na kusimamia misitu kwa njia uendelevu.

## Kusudio la mradi

Kudhihirisha katika ngazi ya kijiji, kitaifa na kimataifa, kwa kutumia njia ya kijamii kupunguza ukataji miti hovyo na uharibifu wa misitu na kutoa motisha yenye usawa kwa jamii zenye usimamizi endelevu wa misitu au kuhifadhi misitu ya Tanzania katika ngazi ya mradi.

http://www.tfcg.org/MakingReddWork.html

## Matokeo ya mradi kwa ufupi


**Tokeo 1: Kuanzishwa kwa ushirika wa jamii wa hewa ukaa.**
MJUMITA itawezeshwa ili ianzishe chombo ambacho kitashughulikia masuala ya hewa ukaa. Muundo wa chombo hiki utahakikisha kuwa motisha inayotolewa kwa ajili ya kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa inayotokana na ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa misitu inawafikia wananchi wa makundi yote wanaoishi katika vijiji vinavyotekeleza mradi.

**Tokeo 2: Upunguzaji wa uharibifu wa misitu sehemu nyingine na kujenga uwezo.**
Kujenga uwezo wa jamii kuzuia uhamishaji wa shughuli zinazochangia uharibifu wa mazingira nje ya eneo la mradi kwa kuanzisha njia mbadala za kujipatia kipato zinazozingatia utunzaji wa mazingira.

**Tokeo 3: Ufuatiliaji, tathmini na mawasiliano.**
Kuwa na mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na mawasilaino ambao utahakikisha kuwa mawasiliano ya matokeo ya mradi katika ngazi ya kijiji na kitaifa yanafanyika kwa ukamilifu.

**Tokeo 4: Uraghibishi katika ngazi ya kitaifa na kimataifa.**
Kuwa na mfumo wa uraghibishi katika ngazi ya kitaifa na kimataifa ambao unaendeleza usawa na ufanisi katika kugawa faida za MKUHUMI hasa kwa watunza misitu katika jamii.






Ramani ya Vijiji vya MKUHUMI vya Kilosa, Mpwampwa na Lindi kuonyesha eneo la Msitu na lisilokuwa la Msitu.

## MKUHUMI kwenye maeneo yenye Bioanuwai nyingi na za kipekee

Mradi unatekelezwa katika Kanda mbili zenye bioanuwai nyingi na za kipekee ambazo ni Kanda ya Misitu ya Pwani na Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki. Kanda hizi ni muhimu sana Kitaifa na Kimataifa kwa sababu zina misitu minene na yenye aina nyingi sana za wanyama na mimea. Wilaya ambazo zinatekeleza mradi huu ni Wilaya ya Lindi ambayo ipo kwenye ukanda wa Misitu ya Pwani na unatekelezwa kwenye vijiji 17. Pia mradi unatekelezwa kwenye Wilaya ya Kilosa ambapo kuna Vijiji 16 na Wilaya ya Mpwapwa ambapo kuna vijiji 6. Wilaya hizi mbili zipo kwenye Misitu ya Millima ya Tao la Mashariki.

## KUHUSU TFCG

Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) lilianzishwa na kusajiliwa kama shirika lisilo la kiserikali mwaka 1985. Shirika lilianzishwa likiwa na maono ya kuhamasisha na kuendeleza uhifadhi wa misitu yenye uwingi wa bioanuwai, iliyoko katika Misitu ya Milima ya Tao la Mashariki na Misitu ya Ukanda wa Pwani Tanzania.

Shirika linafanya kazi katika zaidi ya vijiji 130 katika misitu ya Tao la Mashariki na misitu ya Ukanda wa Pwani.

Miongoni mwa shughuli za TFCG ni Usimamizi Shirikishi wa Misitu; Mawasiliano na Uhamasishaji; Maendeleo ya jamii; Uraghibishi na Utafiti wa bioanuwai.

## KUHUSU MJUMITA

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) ni shirika lisilo la kiserikali, lililoanzishwa mwaka 2000 na kusajiliwa mwaka 2007.

MJUMITA ilianzishwa kwa madhumuni ya kuunganisha jamii zinazoishi pempezoni mwa rasilimali za misitu ili kubadilishana uzoefu kuhusu usimamizi shirikishi wa misitu na kushiriki katika mjadala wa msuala muhimu ya sera zinazohusiana na maliasili.

Kwa sasa MJUMITA ina mitandao ya jamii zaidi ya 80 inayoundwa na kamati za maliasili za vijiji, vikundi vya mazingira na watumiaji wa rasilimali za misitu vijijini. Mtandao huu unahusisha vikundi zaidi ya 500 katika vijiji 320 ambavyo viko katika wilaya 23 Tanzania Bara.

## Kwa Mawasiliano zaidi:

Mkurugenzi Mtendaji TFCG
S.L.P. 23410, Dar es salaam
Simu: +255 22 2669007
Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz
**www.tfcg.org**

Mkurugenzi Mtendaji MJUMITA
S.L.P. 21522, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2669007
Barua pepe: mjumita@googlemail.com
**www.mjumita.org**

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
★ MJUMITA ★

# MKUHUMI KWA AJILI YA JAMII NA MISITU

REDD: FOR COMMUNITIES AND FORESTS
MKUHUMI: KWA AJILI YA JAMII NA MISITU

